**HOTUBA YA MHE. DR. FAUSTIN NDUGULILE (MB), NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO WAKATI WA KUKABIDHIWA CHETI CHA UTOAJI HUDUMA BORA KWA KIWANGO CHA KIMATAIFA (ISO) KWA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA TAREHE 20/08/2018**

- **Mhe. Anne Makinda, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya;**
- **Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya;**
- **Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya,**
- **Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,**
- **Viongozi wa Taasisi na Idara Mbalimbali,**
- **Mwakilishi kutoka BSI,**
- **Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi,**
- **Watumishi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya,**
- **Wanahabari,**
- **Wageni Waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kukutana siku hii muhimu. Pili, niwashukuru watumishi wote wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya mkiongozwa na Bodi pamoja na Menejimenti kwa kuamua kutekeleza jambo hili

muhimu linalolenga kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma bora kwa viwango vya Kimataifa kwa wanachama na wadau wa Mfuko na leo hii nikiongoza kukabidhiwa cheti cha ubora wa huduma cha kimataifa.

Aidha, nimshukuru na kumpongeza pia Mtaalam Mshauri ambaye mmefanya naye kazi hii hatimaye mmeweza kufikia mafanikio haya. Naipongeza Kamati ya Mfuko iliyosimamia jambo hili. Kama mlivyotangulia kusema haikuwa rahisi kwa hiyo najua hata kwenu haikuwa rahisi lakini kwa kushirikiana mmeweza. Hongereni sana.

**Ndugu Wajumbe**, Wakati Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli ilipoingia madarakani, moja kati ya vipaumbele vyake ni wananchi kupata huduma zenye ubora na kwawakati. Leo hii NHIF mmethibitishia kwamba suala hili linawezekana na mlikubali kupita katika mchakato wa kupimwa na Shirika la British Standard Institute (BSI) linalojihusisha na uandaaji na uchapichaji wa viwango vya kimataifa pamoja na utoaji wa vyeti vya huduma bora. Ili kufikia hatua hii ya kukubalika na kutambulika katika utoaji wa huduma bora kimataifa, shirika hulazimika kupita katika mchakato mrefu wa ndani wa kuboresha taratibu za utendaji kazi wake na mazingira ya utoaji huduma kwa washika dau wake, ambao nyinyi mmefikia viwango hivyo. Kwa kweli, nawapongeza sana kwa kazi nzuri.

**Ndugu Wajumbe**, Sisi kama Wizara tunafarijika sana kuona juhudi kubwa zinazofanywa na taasisi hii chini ya Wizara ya Afya za kudhamiria kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma kwa wanachama wa Mfuko na wananchi kwa ujumla. Juhudi hizi zilizofanywa na Bodi, Menejimenti na Watumishi wa Mfuko,

zinafanya idadi ya Taasisi chini ya Wizara ya Afya zilizofanikiwa kutunukiwa cheti cha utoaji wa huduma kwa ubora wa Kimataifa kuongezeka.

**Uboreshaji wa huduma za matibabu nchini:**

**Ndugu Wajumbe,** Serikali imeboreshe hali ya upatikanaji wa dawa nchini kwakuongeza bajeti ya dawa kutoka bilioni 30 2015/16 ilipoingia madarakani na kufikia bilioni 270 mwaka wa fedha 2018/2019 na kufanya hali ya upatikanaji wa dawa kufikia asilimia **90 ya dawa muhimu (essential medicines) katika vituo vyetu vya kutolea huduma hivyo kufanya tatizo la ukosefu wa dawa kupungua kwa kiasi kikubwa sana.** Hivyo, kitendo cha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuthibitishwa katika utoaji wa huduma bora kwa viwango vya Kimataifa kinakwenda sambamba na juhudi hizi za Serikali na hatimaye kuleta matokeo chanya katika utoaji wa huduma kwa wanachama wa Mfuko lakini pia kuwafikia wananchi wengi zaidi.

**Utoaji wa Huduma bora kwa wanachama na wadau wenu:**

**Ndugu Wajumbe,** Kama ambavyo Mkurugenzi Mkuu ametuthibitishia kuwa, Mfuko kwa sasa unatoa huduma kwa wanachama wake na watoa huduma wake kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa, Serikali inaamini viwango hivi havitashuka bali mtaendelea kuvipandisha mwaka hadi mwaka na kuzidi kuboresha huduma na uimarishaji wa matibabu nchini. Viwango hivi mlivyofikia vikawe suluhu ya changamoto ambazo wadau wa Mfuko wamekuwa wakikutana nazo pindi wanapohitaji huduma zitolewazo na Mfuko.

## Azma ya Serikali ya Afya Bora kwa wote:

**Ndugu Wajumbe,** Lengo la Serikali hii ni kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora za matibabu. Tukiwa na lengo la kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anakuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu pindi anapougua pasipo kuwa na kikwazo cha fedha. Ili kutekeleza azma hii, Serikali kupitia Wizara yangu imeweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kila mtanzania anakuwa na bima ya afya hivyo katika utendaji kazi hakikisheni hili mnalizingatia kutokana na mipango mbalimbali mliyojiwekea ya kumfikia kila mwananchi, ikiwa pamoja na kuingiza makundi mbalimbali hususani wakulima kupitia Mpango wa Ushirika Afya naToto kadi.

## Umuhimu wa huduma za afya kwa Watanzania:

**Ndugu Wajumbe,** Katika utekelezaji wa majukumu yenu, tambueni kuwa mnalo jukumu kubwa la kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za matibabu kupitia mfumo wa Bima ya Afya na katika viwango vya utoaji wa huduma mlivyofikia naamini hilo mtalisimamia vizuri na hatimaye lengo la Serikali la Afya Bora kwa wote likawezekana.

Viwango ambavyo mtavitumia katika utoaji wa huduma ni vyema vikaenda sambamba na viwango vya kuwafikia wananchi wengi zaidi ili wajiunge na wanufaike  na huduma za matibabu ambazo mnazitoa. Mimi nimezunguka maeneo mbalimbali ya nchi yetu na nimeona jinsi watu wanavyoteseka kwa sababu ya kushindwa kugharamia huduma za matibabu kwa familia zao na ndio maana

tumekuwa tukiwasukuma sana NHIF kuhakikisha wanawafikia wananchi katika maeneo yote ili kila Mtanzania awe na uhakika wa kupata huduma za matibabu. Endeleeni kuwa wabunifu ili kuwa na vifurushi mbalimbali vya bima ya afya vitakavyowezesha wananchi wengi zaidi kujiunga kwa kuchagua aina ya kifurushi wanachoweza kununua na kunufaika na bima ya afya.

**Hitimisho:**

**Ndugu Wajumbe**, baada ya kusema haya machache sasa nitoe maelekezo mafupi kama ifuatavyo:-

- **Kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**, hakikisheni mnaendelea kuboresha huduma zenu kwa wadau wenu wote kila iitwapo leo ili muweze kukilinda cheti hiki na kuboresha ufanisi katika utoaji huduma zenye viwango hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali imeelekeza juhudi zake kubwa katika kuimarisha sekta ya afya.
- Pili hakikisheni mafanikio haya hayaishii hapa makao makuu bali mujiwekee malengo ya kuhakikisha ofisi zenu zote zinatoa huduma zenye viwango vya kimataifa.

- **Kwa Watoa Huduma**, angalieni namna bora ya kuwahudumia wanachama wa NHIF hasa kwa kushughulikia changamoto za wagonjwa ambao hutumia muda mrefu kusubiri huduma, hivyo, wekeni utaratibu mzuri ambao unapunguza kabisa foleni kwenye vituo vyao katika sehemu zenye changamoto hizo.
-
- Aidha, Wizara imekamilisha na kuzindua mwongozo mpya ya utoaji wa huduma nchini. Hivyo nitumie fursa hii kuwaagiza

watoa huduma wote kuzingatia na kuanza kutumia mwongozo huo wakati wa kutoa huduma kwa wanachama wa NHIF na wananchi kwa ujumla.

- **Kwa wanachama wa Mfuko,** hakikisheni mnazingatia haki na wajibu wenu wakati wa kupata huduma za matibabu katika vituo vya kutolea huduma. Zama hizi ni za uwazi na ziko njia nyingi za mawasiliano. Usisite kutujulisha endapo kuna mahali unaona haki yako haizingatiwi.

- **Kwa wananchi,** Niwaombe wananchi wote ambao hamjajiunga na huduma za Mfuko mtumie fursa hii kujiunga sasa ili muwe na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wowote., suala la bima ya afya ni la msingi na haliepukiki endapo mtu anahitaji kuwa na uhakika wa kupata huduma wakati wowote.

Baada ya kusema haya, nirejee kuipongeza Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti na watumishi wote wa Mfuko pamoja na kuwashukuru kwa kunialika katika tukio hili muhimu sana kwa maendeleo ya utoaji wa huduma bora kwa wanachama. Sasa niko tayari kupokea cheti cha utoaji wa huduma kwa kiwango cha kimataifa.

**Asanteni kwa kunisikiliza**.